JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

04 **HISABATI**

Muda: Saa 2:00 **Jumatano, 05 Septemba 2018 asubuhi**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45).**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Soma maelekezo yote yaliyoko katika **fomu maalum ya kujibia (OMR).**
4. Jaza taarifa zote katika fomu ya OMR na katika ukurasa wenye swali la 41 hadi 45 kwenye karatasi ya maswali.
5. Weka **kivuli** katika kila tarakimu ya **Namba yako ya Mtihani** kwenye nafasi husika katika fomu ya OMR.
6. Kokotoa na kisha **weka kivuli** kwenye herufi ya jibu lililo sahihi kwa swali la 1 - 40. Kwa mfano, kama jibu sahihi ni A weka kivuli kama ifuatavyo:

~~[A]~~	[B]	[C]	[D]	[E]

7. Ukigundua kuwa herufi uliyowekea kivuli **si jibu sahihi,** futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia **kifutio safi** kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
8. Tumia **penseli ya HB** tu katika kujibu swali la 1 hadi 40; na kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi** kwa swali la 41 hadi 45.
9. Onesha wazi njia iliyotumika katika kujibu swali la 41 hadi la 45.
10. Simu za mkononi, vikokotozi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

1 807004 100014

Scanned with CamScanner

SEHEMU A: MATENDO YA KIHISABATI, MAUMBO NA MAFUMBO

Katika swali la 1 – 40, kokotoa swali ulilopewa na kisha weka kivuli kwenye herufi ya jibu lililo sahihi katika fomu yako ya kujibia.

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
1.	$1,236 \div 4 =$ A 39 B 309 C 63 D 306 E 49.	
2.	Andika $\left(\frac{7}{12} + \frac{2}{12}\right)$ katika sehemu rahisi. A $\frac{3}{4}$ B $\frac{9}{12}$ C $\frac{9}{24}$ D $\frac{3}{8}$ E $\frac{2}{12}$.	
3.	$269 + 1,731 =$ A 1,800 B 1,900 C 1,990 D 1,999 E 2,000.	
4.	$4\frac{4}{5} \div 1\frac{1}{5} =$ A 2 B 3 C 4 D 5 E 6.	
5.	$1,509 - 728 =$ A 581 B 681 C 771 D 781 E 881.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
6.	$7\frac{3}{5}-2\frac{1}{2}=$ A 3 B $3\frac{2}{5}$ C $3\frac{1}{10}$ D $4\frac{1}{10}$ E $5\frac{1}{10}$.	
7.	$78\times952=$ A 74,256 B 70,756 C 74,246 D 74,156 E 73,856.	
8.	Ikiwa $p=5$ na $Q=4$, tafuta thamani ya $(P^2)\times(Q^2)$ A 54 B 108 C 400 D 200 E 800.	
9.	Bwana Matata alizaliwa mwaka 1961. Andika mwaka huo kwa namba za kirumi. A MMCLXI B MCMLXI C MCMXLI D MCMCXI E MXMLXI	
10.	$1.9-0.06=$ A 0.94 B 1.94 C 1.86 D 1.84 E 1.96.	
11.	Badili 44% kuwa sehemu rahisi. A $\frac{44}{100}$ B $\frac{22}{25}$ C $\frac{11}{50}$ D $\frac{22}{50}$ E $\frac{11}{25}$.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
12.	Tafuta thamani ya 49^2. A 2,401 B 2,301 C 1,301 D 98 E 492.	
13.	$3-(6-^-8)=$ A 17 B -1 C -11 D 1 E 11.	
14.	Je, kuna namba shufwa ngapi kati ya 73 na 81? A 7 B 6 C 5 D 4 E 3.	
15.	Zidisha kg 8 gm 50 kwa 5. A kg 40 gm 25 B kg 40 gm 250 C kg 42 gm 250 D kg 42 gm 225 E kg 40 gm 455.	
16.	Andika namba inayokosekana katika mfululizo wa namba ufuatao: 70, 85, 100, ..., 130. A 101 B 105 C 108 D 110 E 115.	
17.	Ikiwa $7m-\frac{1}{3}=2$, tafuta thamani ya m. A $\frac{2}{3}$ B $\frac{7}{3}$. C $\frac{2}{7}$ D $\frac{1}{3}$ E $\frac{1}{7}$.	

CC-18/7SE

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
18.	Tafuta Kigawo Kikubwa cha Shirika (KKS) cha 32 na 48. A 16 B 12 C 8 D 4 E 2.	
19.	$15.65 \times 12 =$ A 31.3 B 15.65 C 187.8 D 178.7 E 187.7.	
20.	$1\frac{4}{5} \times 3\frac{8}{9} =$ A $3\frac{1}{7}$ B 7 C $\frac{44}{14}$ D 8 E $4\frac{12}{14}$.	
21.	Tafuta kipeuo cha pili cha (64×4). A 4 B 8 C 16 D 32 E 64.	
22.	Ikiwa $M = -3$ na $N = -5$, tafuta thamani ya $(-9 \times M \times N)$. A −105 B 15 C -125 D −135 E 135.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
23.	Tafuta eneo la umbo lifuatalo:  A sm^2 80 B sm^2 40 C sm^2 21 D sm^2 20 E sm^2 160.	
24.	Andika majira ya nukta P na Q.  A P(2, -3) Q(2, 0) B P(-3, 2) Q(0, -2) C P(2, 3) Q(-2, 0) D P(2, -3) Q(0, -2) E P(0, -2) Q(2, -3).	

CC-18/PSLE

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
25.	Tafuta ukubwa wa pembe ABC katika umbo lifuatalo:  A 50° B 60° C 65° D 70° E 90°.	
26.	Mzingo wa duara lifuatalo ni sm 352. Tafuta nusu kipenyo cha duara hilo. (Tumia $\pi = \frac{22}{7}$).  A sm 28 B sm 44 C sm 56 D sm 88 E sm 176.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Schemu ya Kazi
27.	Tafuta thamani ya x katika mchoro ufuatao:  A 90^0 B 60^0 C 45^0 D 40^0 E 30^0.	
28.	Tafuta eneo la umbo lifuatalo:  A sm^2 144 B sm^2 124 C sm^2 120 B sm^2 64 E sm^2 36.	
29.	Tafuta mzingo wa pembetatu pacha PQR.  A sm 10 B sm 38 C sm 18 D sm 24 E sm 14.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
30.	Tafuta ukubwa wa umbo lifuatalo:  A sm^3 192 B sm^3 224 C sm^3 128 D sm^3 256 E sm^3 64.	
31.	Tafuta eneo la umbo lifuatalo:  A sm^2 30 B sm^2 24 C sm^2 40 D sm^2 48 E sm^2 60	
32.	Joni alinunua maembe 225 kwa mkulima. Aliuza maembe 135 kwa siku moja. Je, maembe aliyouza ni asilimia gani ya maembe yote. A 20 % B 30% C 40 % D 51 % E 60 %.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi
33.	Jumla ya urefu wa pande sambamba za trapeza ni sm 24. Ikiwa kimo cha trapeza ni sm 7, tafuta eneo la trapeza hiyo. A sm^2 72 B sm^2 74 C sm^2 82 D sm^2 84 E sm^2 158.	
34.	Martha hutembea kwa mwendokasi wa kilometa 2 kwa saa kutoka nyumbani hadi dukani. Ikiwa hutumia nusu saa, je, ni umbali gani kutoka nyumbani hadi dukani? A km 1 B km 2 C km 3 D km 4 E km 5.	
35.	Vijiji vinne katika mkoa mmoja vilivuna korosho kilogramu 60,000. Je, kwa wastani kila kijiji kilivuna tani ngapi? (Tani moja = Kilogramu 1,000). A tani 5 B tani 10 C tani 15 D tani 20 E tani 25.	
36.	Mkulima aliuza pamba na kupata shilingi 2,500,000. Ikiwa mauzo kwa kilo moja ni shilingi 2,500, je, aliuza kilo ngapi? A 25 B 50 C 500 D 1,000 E 1,500.	

Scanned with CamScanner

Na.	Swali	Schemu ya Kazi
37.	Jumla ya umri wa baba na mtoto ni miaka 40. Ikiwa umri wa baba ni mara tatu ya umri wa mtoto, je, mtoto ana umri wa miaka mingapi? A 5 B 10 C 15 D 20 E 25.	
38.	Idadi ya wanafunzi wa Darasa la 5B katika shule ya msingi Mwembeni waliofaulu katika jaribio la kila wiki la somo la Hisabati kwa wiki nne ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo: Wiki | I | II | III | IV Idadi ya Wanafunzi | 76 | 64 | ... | 72 Ikiwa wastani wa idadi ya wanafunzi waliofaulu ni 70, je wiki ya tatu walifaulu wanafunzi wangapi? A 64 B 66 C 68 D 70 E 72.	
39.	Shule ya msingi Mapinduzi ina jumla ya wanafunzi 860. Ikiwa wavulana ni 432, je, wasichana ni wangapi? A 328 B 418 C 432 D 438 E 428.	
40.	Dawati moja katika chumba cha Darasa la Sita hukaliwa na wanafunzi 3. Ikiwa chumba cha Darasa hilo kina wanafunzi 60, je, kina madawati mangapi? A 20 B 30 C 40 D 50 E 60.	

Scanned with CamScanner

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI SEPTEMBA 2018

04 **HISABATI**

Jaza taarifa zako kwa usahihi katika nafasi zilizo wazi. Tumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

Mkoa_____ **Wilaya**_____

Shule_____

Namba ya Mtahiniwa_____

SEHEMU B: MATENDO YA NAMBA, MAUMBO NA MAFUMBO

Katika swali la 41 – 45, kokotoa swali ulilopewa kwa kutumia **kalamu ya wino wa bluu au mweusi** kisha andika majibu kwenye nafasi iliyotengwa.

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
41.	$(^{-}12 - ^{-}3) \times (^{-}6 - ^{-}3) =$		
42.	Kidawa hutumia mshahara kama inavyooneshwa katika grafu kwa duara. Iwapo mshahara wake ni sh 720,000. je hutenga kiasi gani kwa mengineyo.  		

1 807004 100014

Scanned with CamScanner

Na	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
43.	Umbo ABCD ni mraba wenye duara lenye kipenyo cha sm 42. Tafuta eneo la sehemu iliyotiwa kivuli. Tumia $\left(\pi = \frac{22}{7}\right)$.  		
44.	Kamota alinunua kilogramu 74.6 za unga wa ngano siku ya kwanza. Siku ya pili alinunua kilogramu 9.53. Je, jumla alinunua kilogramu ngapi kwa siku mbili?		
45.	Mwanahawa alinunua vitu vifuatavyo: Magodoro 6 @ sh 80,000 Viti 10 @ sh 20,000 Meza 5 @ sh 40,000 Je alibakiwa na kiasi gani cha fedha ikiwa alikuwa na sh 1,000,000 mfukoni.		
	Jumla ya Alama		
	Sahihi ya Mhakiki		

Scanned with CamScanner